

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA
Barua zote ziandikwe kwa: Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,



Simu Na 023 2402738,
Fax Na 023 402706
Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P. 10,
MKURANGA,
PWANI.

17/12/2020

Kumb. Na. LD/MK/6561/26
Mkurugenzi Mkuu,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P.938,

Dar es salaam

**YAH: KUITAMBULISHA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA KAMAKA IT
SOLUTION KUPATA ARDHI, WILAYANI MKURANGA**

Rejea mada tajwa hapo juu.

Ninachukua fursa hii kuijulisha Ofisi yako kwamba, Kampuni tajwa hapo juu imepata Ardhi ambayo imeandaliwa Mpango wa matumizi na kupimwa na kuwa **kiwanja Na.30 Kitalu B Kisemvule**, yenye ukubwa wa **mita za mraba 16,188** kwa matumizi ya Kiwanda.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999, fungu la 19-20 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na.26 ya mwaka 1997, aidha kwa kuzingatia fungu la 12 na 179 Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 na Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, kanuni za Ardhi za 2001, kanuni ya 9C(v), kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi kwako ili iweze kupatiwa Certificate of Incentive yenye kuonyesha namba ya kiwanja uwekezaji utakapofanyika ili kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya kuandaa Designation for Investment-Land form Na.1 ili kiwanja hiki kitangazwe kuwa cha Uwekezaji na hatimaye kuingizwa katika kamati ya Ugawaji wa Ardhi Taifa.

Tunawasilisha taarifa hii kwako ili kuiwezesha Kampuni hii kupata hati hiyo ya Utambulisho ambayo ni kiambatanisho muhimu katika uwasilishaji wa taarifa Wizara ya Ardhi kitengo cha Uwekezaji kwa ajili ya umilikishaji wa ngazi ya Taifa, naambatanisha nyaraka za usajili wa Kampuni, mkataba wa kupata Ardhi, MoU and Article of Association, ramani ya Mipango Miji na ramani ya Upimaji kwa ajili ya kumbukumbu za ofisi.

Nawasilisha kwako kwa hatua zaidi.

Eng. Mshamu A. Munde
Mkurugenzi Mtendaji (W),
Mkuranga.

